BENKI KUU YA TANZANIA

# UCHUMI WETU

## TOLEO NA. 03, JANUARI 2026








# KUTOKA MEZA YA GAVANA



**Kheri ya mwaka mpya 2026**

Kwa mara nyingine tena, ninayo furaha kuwakaribisha wasomaji wote katika jarida la UCHUMI WETU, toleo la tatu. Jarida hili linawapa taarifa na uelewa wa masuala mbalimbali ya uchumi na sera za fedha, yanatekelezwa na taasisi za fedha ndani na nje ya nchi yetu.

Kabla ya kugusia machache yaliyopo kwenye jarida hili, napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kingine, pamoja na Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha pili. Vile vile, nampongeza kwa dhati aliyekuwa Waziri wetu wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatakia kila la heri viongozi wetu hawa katika utekelezaji wa majukumu yao, yenye lengo la kukuza uchumi na ustawi wa watanzania.

Napenda pia kumpongeza Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akirithi mikoba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu wa sasa. Nawapongeza pia Manaibu Waziri wake ambao ni Mhe. Laurent Deogratius Luswetula na Mhe. Mhandisi Mshamu Munde. Kwa upande wa Zanzibar, napenda kutumia fursa hii pia kumpongeza Mhe. Dkt. Juma Malik Akil kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha. Tunaahidi kuwapa viongozi wote hawa ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

Ndugu wasomaji wetu, ninayo furaha kuwajulisha kuwa mwenendo wa uchumi wa nchi yetu umeendelea kuwa mzuri kama inavyoonekana kwenye taarifa na machapisho mbalimbali ya Benki Kuu, ikiwemo Taarifa ya Kamati ya Sera ya Fedha ya Januari 2026. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa takriban asilimia 5.9 mwaka 2025, ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6, na uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 6.8 kwa mwaka 2025.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Katika robo ya nne ya mwaka 2025, mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara ulikuwa wastani wa asilimia 3.5, na kwa upande wa Zanzibar ulikuwa asilimia 3.4. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 20.3 katika robo ya nne ya mwaka 2025 hali inayoonesha kuimarika kwa mazingira ya biashara na kuongezeka kwa imani ya sekta binafsi katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi nchini.

Sekta ya benki imeendelea kuwa imara, ikiwa na ukwasi wa kutosha unaowezesha utoaji wa mikopo, na mtaji wa kutosha unaohimili misukosuko ya kiuchumi. Aidha, vihatarishi katika utoaji wa mikopo vimeendelea kupungua ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulifikia asilimia 3.1 katika robo ya nne ya mwaka 2025, ikiwa ni chini ya ukomo wa kiwango kinachovumilika cha asilimia 5. Vile vile, mifumo ya malipo imeendelea kuwa thabiti, ikifanya kazi kwa ufanisi mzuri mijini na vijijini.

Sekta ya nje imeendelea kuimarika, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inakadiriwa kupungua hadi asilimia 2.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025, ikiwa ni kiwango cha chini zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Aidha, ukwasi wa fedha za kigeni ulikuwa wa kutosha na thamani ya shilingi imeendelea kuwa tulivu dhidi ya sarafu nyingine. Hadi mwezi Desemba 2025, akiba ya fedha za kigeni ilifikia zaidi ya dola bilioni 6.3, kiasi kinachokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi 4.9, ikiwa ni juu ya lengo la angalau miezi 4.

Katika toleo hili la Jarida la UCHUMI WETU, mtajionea mafanikio ambayo Benki Kuu imeyapata katika programu yetu ya ununuzi wa dhahabu nchini, namna Benki Kuu ilivyoshiriki katika mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa yenye tija kwa taifa letu, namna Benki Kuu ya Tanzania inavyoshirikiana na Benki Kuu za nchi nyingine katika kubadilishana ujuzi na maarifa, na mchango wa Benki Kuu ya Tanzania kwenye mafunzo ya kuwandaa vijana kuitumikia sekta ya fedha kwa ufanisi na kufanya maamuzi sahihi katika usimamizi binafsi wa kifedha.

Aidha, toleo hili linaainisha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika sekta ya fedha ikiwemo malipo ya fidia kwa wateja wa iliyokuwa Benki ya FBME, maendeleo kwenye soko la hisa na hatifungani, na mabadiliko chanya kwenye sekta ya bima. Vile vile, toleo hili linagusia mikakati mbalimbali ya Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, kwa lengo la kufikia azma ya Dira ya Taifa 2050.

Katika toleo hili pia utapata fursa ya kuelimishwa kwa kina juu ya umuhimu wa kutumia mifumo ya malipo ambayo husimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, kwani ni njia rahisi na salama ya kufanya miamala wakati wote. Benki Kuu imekuwa ikihakikisha Mifumo ya Malipo ya Taifa inakuwa imara na thabiti kwa kuendana na teknolojia ya kisasa ili kuongeza ufanisi.

Mifumo ya malipo ya Taifa ina faida kubwa kwa uchumi wa nchi, na kwa taasisi au watu binafsi wanaopokea na kutoa huduma nchini. Kupitia mifumo hii, ni rahisi kufahamu kwa usahihi kiasi cha fedha kilichopo kwenye mzunguko wa uchumi, jambo linalosaidia katika kupanga na kusimamia sera za fedha. Aidha, mifumo hii humsaidia mtumiaji binafsi kufuatilia matumizi yake, kuweka mipango ya kifedha ya muda mfupi na mrefu, pamoja na kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha, kwani wakati wote anakuwa anajua mwenendo wa mapato na matumizi yake.

Napenda kusisitiza kuwa mifumo yetu ya malipo ina uthabiti wa hali ya juu na viwango madhubuti vya usalama, hivyo kuwalinda watumiaji dhidi ya hatari za upotevu wa fedha na matumizi yasiyo halali. Benki Kuu itaendelea kuboresha mifumo hii ili iendane na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya uchumi unaokua kwa kasi duniani.

Vile vile, katika toleo hili tumeonesha namna watumishi wa Benki Kuu wanavyoshirikiana na jamii inayowazunguka kwa kutoa elimu na misaada mbalimbali, ambapo watumishi wa Tawi la Dodoma wamejenga jengo la jiko katika kituo cha watoto yatima cha Qadriya, Dodoma. Hivyo, tutaendelea na jitihada hizi kwa kadri itakavyowezekana.

Napenda kuhitimisha kwa kuwakaribisha tena kusoma toleo letu hili la tatu la jarida la UCHUMI WETU. Ninaamini tutapata taarifa na maarifa ya kutosha kupitia jarida hili kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Nawatakia wote kheri ya mwaka mpya na usomaji mwema.

**Emmanuel Mpawe Tutuba**
Gavana, Benki Kuu ya Tanzania.

# KUTOKA MEZA YA MHARIRI MKUU



**Ndugu Msomaji wetu,**

Karibu katika jarida la Uchumi Wetu toleo la tatu. Jarida hili litakuelimisha na kukupatia taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya uchumi na sekta ya fedha nchini, hususani yale yanayoratibiwa na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa sheria. Katika toleo hili, utapata taarifa kwa kina kuhusu shughuli na majukumu ya Benki Kuu Ya Tanzania (BOT) katika kuratibu na kusimamia sekta ya fedha na uchumi wa nchi kiujumla.

Miongoni mwa habari tulizokuandalia katika jarida hili ni pamoja na Gavana wa Benki Kuu awataka wafanyakazi wa sekta ya fedha nchini kuwa wazalendo na kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uadilifu. Vilevile utaelimishwa kwa kina namna mifumo ya malipo ya Taifa inavyowezesha ulipaji malipo mbalimbali kwa ufanisi mkubwa.

Kwa kushirikiana na wadau wetu mbalimbali, utapata fursa ya kupata habari na taarifa kutoka kwa taasisi za fedha nchini ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji na Dhamana nchini (CMSA), Bodi ya Bima ya Amana nchini (DIB), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Katika kujenga ushirikiano na jamii inayotuzunguka, Benki Kuu hutumia fursa mbalimbali zinazojitokeza kutoa elimu kwa Umma kuhusu majukumu inayotekeleza, kupokea maoni na ushauri mbalimbali toka kwa wadau wetu kwa minajili ya kuzidi kuboresha zaidi huduma zetu.

Ni matumani yangu kuwa, kupitia jarida hili utapata fursa ya kuielewa sekta ya Uchumi na Fedha kupitia makala, vibonzo, habari picha na mashairi yaliyomo katika Jarida letu Uchumi wetu Toleo la 3.

Endapo una maoni, ushauri au mapendekezo yoyote, tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: **botcommunications@bot.go.tz**

Nakutakia usomaji mwema.

**Victoria Msina**
Meneja, Idara ya Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania.

# BENKI KUU YA TANZANIA

# 2026

## HERI YA MWAKA MPYA

Ninaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwatakia Heri ya Mwaka Mpya wadau wa Benki Kuu ya Tanzania pamoja na watanzania wote.

Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kusimamia uthabiti wa sekta ya fedha na uchumi kwa kutekeleza sera madhubuti zitakazodhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha thamani ya shilingi, na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi kwa maendeleo ya Taifa.

Tuendelee kulinda amani, kuimarisha umoja, na kujenga kwa vitendo mustakabali wa matumaini ya Taifa letu.



Emmanuel M. Tutuba
**Gavana**

# RIBA YA BENKI KUU YASALIA ASILIMIA 5.75



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, akizungumza wakati alipotangaza riba ya Benki Kuu kwa robo ya kwanza ya mwaka 2026 katika mkutano na waandishi wa habari pamoja na viongozi wa mabenki na taasisi za fedha uliofanyika tarehe 8 January 2026, katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeamua kuendelea na kiwango cha Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate – CBR) cha asilimia 5.75 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2026, kiwango ambacho kilitumika pia katika robo ya nne ya mwaka 2025.

Uamuzi huo ulitangazwa Januari 8, 2026 na Gavana wa BoT na Mwenyekiti wa Kamati ya Sera ya Fedha, Bw. Emmanuel Tutuba, wakati wa mkutano na viongozi wa benki, taasisi za fedha pamoja na waandishi wa habari.

Akizungumza katika mkutano huo, Gavana Tutuba alisema uamuzi wa kubakiza CBR umefikiwa baada ya tathmini ya kina ya hali ya uchumi wa ndani na wa dunia.

"Uamuzi huu umezingatia matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Kuendelea kubakiza kiwango cha CBR kama kilivyokuwa katika robo ya nne ya mwaka 2025 kutasaidia kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kuwezesha uchumi wa taifa kuendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha," alisema.

Alifafanua kuwa kiwango cha Riba cha Benki Kuu ni kiwango kinachowekwa na BoT kama rejea katika utekelezaji wa shughuli zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukopesha benki za biashara. Kiwango hiki huathiri riba za mikopo baina ya benki za biashara, ambazo zinapaswa kuwa ndani ya wigo wa ±2.0% ya riba ya Benki Kuu iliyowekwa.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa ndani, Gavana Tutuba alisema uchumi wa Tanzania Bara uliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha ya takriban asilimia 5.9 mwaka 2025, ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 6. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, madini na ujenzi.



Kwa upande wa Zanzibar, alisema uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 6.8 mwaka 2026, ukichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, utalii na uzalishaji viwandani.

Katika hatua nyingine, Gavana Tutuba aliwapongeza wadau wa sekta ya fedha kwa jitihada zao zilizopelekea kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu hadi kufikia asilimia 3.1, kiwango kilicho chini ya ukomo unaovumilika wa asilimia 5.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki nchini, Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Bw. Herman Kasekende, aliipongeza Benki Kuu ya Tanzania kwa usimamizi thabiti wa sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla.

Alisema usimamizi huo umechangia kuimarika kwa sekta ya kibenki, kudhibiti mfumuko wa bei, kudumisha utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za kigeni, pamoja na kuwepo kwa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni.



# MUHTASARI WA TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA KWA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2026

**08 JANUARI 2026**

**RIBA YA BENKI KUU KWA ROBO YA KWANZA YA 2026 KUBAKIA 5.75%**




### UKUAJI WA UCHUMI
Katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, uchumi wa Tanzania bara unatarajiwa kukua kwa 6% na wa Zanzibar kwa 7.2%

### URARI WA MALIPO YA KAWAIDA
**Tanzania Bara:**
Unakadiriwa kupungua hadi 2.2% ya Pato la Taifa (GDP) kwa mwaka 2025.

**Zanzibar:**
Imeendelea kuwa zaida katika urari wa malipo ya kawaida, ikichangiwa zaidi na mapato yatokanayo na sughuli za utalii.

### SEKTA YA KIBENKI
Uwiano wa mikopo chechefu (NPLs) ulipungua na kufikia 3.1%, chini ya ukomo unaovumilika wa 5%

### MFUMUKO WA BEI
Katika robo ya nne ya mwaka 2025, kwa Tanzania Bara ulikua wa wastani wa 3.5% na kwa upande wa Zanzibar ulikua 3.4%.

### AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI
Ilifikia zaidi ya dola bilioni 6.3, kiasi kinachoweza kufanya uagizaji wa bidhaa wa huduma kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi 4.9.

### UTEKELEZAJI WA SERA YA BAJETI
Tathmini ya uhimilivu wa deni kwa 2024/25 inaonesha uwiano wa deni la umma kwa Pato la Taifa ulipungua hadi 40.6% kutoka 41.1% mwaka 2023/24.

# BOT YAFIKISHA TANI 15.37 ZA DHAHABU



Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda, alipotembelea ofisi za Mkuu Mkoa huyo katika ziara ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu iliyofanyika tarehe 26 Novemba 2025.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amesema kuwa hadi sasa Benki Kuu imenunua jumla ya tani 15.37 za dhahabu kupitia mpango wake wa ununuzi wa madini hayo, ikiwa ni hatua muhimu ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi.

Kauli hiyo aliitoa wakati wa ziara ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu katika mikoa ya Mwanza na Geita tarehe 26 Novemba 2025, ziara iliyoongozwa na Mwenyekiti wa Bodi hiyo ambaye pia ni Gavana.

Katika hatua ya kwanza ya ziara hiyo, Bodi ilitembelea ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda, ambaye alieleza kuwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati unaendelea vizuri, ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na ujenzi wa jengo la abiria na mizigo katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Alisema kukamilika kwa miradi hiyo kutaimarisha mchango wa Mkoa wa Mwanza katika pato la taifa.

Aidha, Mhe. Mtanda alibainisha kuwa kukamilika kwa Daraja la J.P. Magufuli pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya meli kubwa katika Ziwa Victoria kumechochea ukuaji wa biashara kati ya Mkoa wa Mwanza na nchi jirani ya Uganda.

Katika Mkoa wa Geita, Bodi ilipokelewa na Kaimu Mkuu wa Mkoa, Mhe. Hashim Komba, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Geita. Mhe. Komba aliipongeza Benki Kuu kwa utekelezaji mzuri wa mpango wa ununuzi wa dhahabu pamoja na ushiriki wake katika Maonesho ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yanayofanyika kila mwaka mkoani humo. Alisema hatua hizo zimeongeza ufanisi katika usimamizi wa sekta ya madini na kuchochea maendeleo ya wachimbaji wadogo na wa kati.

Vilevile, Bodi hiyo ilipata fursa kutembelea Soko la Madini la Mwanza pamoja na Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu cha Mwanza Precious Metals Refinery. Ziara iliendelea hadi Geita, ambako Bodi ilitembelea Soko la Madini la Geita na Kiwanda cha Geita Gold Refinery, na kupata maelezo kuhusu mwenendo wa biashara ya madini na maendeleo ya teknolojia za uchakataji dhahabu katika maeneo hayo.

Ziara hii imetoa nafasi muhimu ya kufuatilia mwenendo wa miradi ya kimkakati pamoja na kujionea moja kwa moja mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa taifa.





# BOT YAENDELEZA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA MIKUTANO YA IMF, BENKI YA DUNIA



Gavana Emmanuel Tutuba (katikati) pamoja na uongozi wa Benki ya Viwanda na Biashara ya China (ICBC) baada ya kikao kilichofanyika katika ofisi za ubalozi wa Tanzania, jijini Washington D.C.,Marekani. Kushoto kwake ni Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, pamoja na Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, walishiriki Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB) iliyofanyika jijini Washington D.C., Marekani kuanzia tarehe 13 hadi 18 Oktoba 2025.

Katika mikutano hiyo, Gavana Tutuba alifanya mazungumzo na viongozi wa Benki ya Viwanda na Biashara ya China (ICBC), akiwemo Mkurugenzi Mtendaji Bw. Peter Poon na Mkurugenzi wa Muundo wa Masoko ya Kimataifa Bi. Yoyo Ye.

Mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha ushirikiano kati ya BoT na ICBC, hususan katika eneo la uhifadhi wa akiba ya taifa. Viongozi hao walijadili fursa za uwekezaji kupitia ununuzi na uhifadhi wa dhahabu, hatua inayotarajiwa kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha nchini Tanzania.

Aidha, Gavana Tutuba alishiriki Mkutano wa 52 wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika (Africa Group 1 Constituency Policy Dialogue), uliofanyika pembezoni mwa mikutano hiyo. Mkutano huo ulihusisha Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu kutoka nchi 14 wanachama wa IMF, akiwemo Tanzania.

Makubaliano yaliyofikiwa yalilenga kuimarisha mikakati ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi na kuongeza mapato ya ndani ili kukabiliana na kupungua kwa mikopo na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Tanzania ilitajwa kufanya vizuri katika kuongeza uwazi wa bajeti na ukusanyaji wa mapato ya ndani, huku ikitekeleza mageuzi ya mifumo ya kodi na matumizi ya teknolojia za kidijitali.




Gavana Emmanuel Tutuba akijadili jambo na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Mwamba, waliposhiriki Mkutano wa 52 wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika, kando Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB) iliyofanyika jijini Washington D.C., Marekani kuanzia tarehe 13 hadi 18 Oktoba 2025.



Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, akijadili jambo na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Amina Shabaan, walipohudhuria kikao cha Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi na Fedha katika Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (MEFMI), kando Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB) iliyofanyika jijini Washington D.C., Marekani kuanzia tarehe 13 hadi 18 Oktoba 2025.

Kwa upande wake, Dkt. Kayandabila alishiriki kikao cha Taasisi ya Usimamizi wa Uchumi na Fedha katika Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (MEFMI), kilichojadili fursa na changamoto za matumizi ya Akili Unde (AI) katika uchumi.

Majadiliano yalijikita katika namna AI inavyoweza kusaidia ukusanyaji wa mapato, uchambuzi wa data kwa ajili ya maamuzi ya kisera, na usimamizi wa huduma za kifedha.

Hata hivyo, changamoto kama uhaba wa wataalamu, miundombinu duni, na masuala ya usalama wa taarifa zilitambuliwa kama vikwazo vinavyohitaji kushughulikiwa.

Ushiriki wa viongozi hawa wa BoT katika mikutano hiyo ni ishara ya dhamira ya Tanzania kuendelea kushirikiana na taasisi za kimataifa katika kuimarisha uchumi wa taifa, kukuza uwazi wa bajeti, na kuongeza mapato ya ndani kupitia sera madhubuti na matumizi ya teknolojia za kisasa.

# AACB YAJADILI ATHARI ZA TABIANCHI NA UTULIVU WA UCHUMI MKUU



Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, katika Mkutano wa 47 wa Mwaka wa Chama cha Mabenki Kuu ya Afrika (AACB) uliofanyika mjini Yaoundé, Cameroon.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dkt. Yamungu Kayandabila, alihudhuria Mkutano wa 47 wa Mwaka wa Chama cha Mabenki Kuu ya Afrika (AACB) uliofanyika mjini Yaoundé, Cameroon.

Mkutano huo uliokuwa na kaulimbiu "Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Utulivu wa Uchumi Mkuu: Jukumu la Benki Kuu" na kuongozwa na Mwenyekiti wa kikao, Gavana wa Benki Kuu ya Mauritius, Dkt. Priscilla Muthoora Thakoor ulifanyika Novemba 28, 2025.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kongamano hilo, Gavana wa Benki ya Mataifa ya Afrika ya Kati (BEAC), Yvon Sana Bangui, alibainisha kuwa mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa changamoto halisi inayozikabili mamlaka za fedha.

"Athari zake zinaonekana moja kwa moja katika uchumi, mifumo ya fedha, na uthabiti wa mataifa, hivyo benki kuu zina wajibu wa kujumuisha hatari hizo katika sera, mifumo ya uchumi mkuu, na vyombo vya kulinda utulivu wa kifedha,"alisisitiza Gavana Bangui

Mada kuu ya mkutano ilikuwa kupitia maendeleo yaliyopatikana chini ya Mpango wa Ushirikiano wa Kifedha wa Afrika (AMCP), ambao ni msingi muhimu unaoongoza safari ya bara hilo kuelekea muunganiko na utangamano wa kifedha.

Aidha, Magavana walijadili uharakishaji wa kuanzishwa kwa Taasisi ya Fedha ya Afrika, wakaidhinisha programu ya kazi ya mwaka 2026–2028 ya Jumuiya ya Wasimamizi wa Benki za Afrika, na kujadili mbinu za kuimarisha ushirikiano wa mifumo ya malipo kwa kutumia miundombinu ya kitaifa na kikanda.

Mkutano huo wa ngazi ya juu uliofanyika tarehe 28 Novemba 2025, ulihitimisha mfululizo wa vikao vya kiufundi pamoja na Kongamano la Magavana, na kuwakutanisha viongozi wa benki kuu, watunga sera, na washirika wa kimataifa lengo likiwa kuendeleza ajenda ya ushirikiano wa kifedha barani Afrika.



# BOT: MIFUMO YA MALIPO YA TAIFA IPO SALAMA



Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imewataka Watanzania na watumiaji wa mifumo ya malipo kuendelea kutumia njia hiyo kwani ni salama na inadhibitiwa kwa teknolojia ya hali ya juu.

Hayo yalielezwa kwa nyakati tofauti na Meneja Msaidi wa Kurugenzi ya Mifumo ya Malipo ya Taifa BoT, Bw. Fabian Kasole wakati akifanya mahojiano na vyombo mbalimbali vya habari Desemba 2025.

Mfululizo wa mahojiano hayo yalifanyika ikiwa ni kampeni maalumu ya kukuza uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia mifumo katika kutuma, kupokea na kufanya malipo.

"Niwahakikishie Watanzania kuwa mifumo ya malipo nchini ipo salama na fedha zenu zipo salama. Mifumo ipo salama ndio maana kuna utulivu kwenye sekta ya fedha, ni wajibu wa Benki Kuu kuhakikisha mifumo ipo salama kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kufanya ukaguzi kwa taasisi hizi za fedha mara kwa mara ili kuikagua mifumo yao,"alisema Kasole

Bw. Kasole alisema ni salama zaidi kutumia mifumo ya malipo kwa sababu inasimamiwa na kudhibitiwa kwa teknolojia ya hali ya juu huku akisisitiza kuwa fedha haiwezi kupotea kwa njia hiyo.

"Katika matumizi ya mifumo ya malipo suala la fedha yako kuchepushwa halipo kabisa, unayemtumia fedha ndio anayepokea. Mfumo hauwezi kukosea kumtumia mtu tofauti na uliyemkusudia labda ukosee wewe,"aliongeza Bw. Kasole.

Mbali na suala la usalama wa mifumo hiyo, pia inasaidia katika kupanga matumizi sahihi ya fedha kwa kuwa unabaki na kumbukumbu ya miamala.

"Ukitumia mifumo ya malipo unabaki na kumbukumbu ya miamala yako na kujua namna bora ya kufanya mipangilio ya matumizi bora ya fedha, pia uchumi wa fedha unahitaji mzunguko wa haraka wa fedha, unavyotumia fedha taslimu unachelewesha mzunguko wa ile fedha,"alisema,

Kuhusu jukumu hilo la kusimamia mifumo, BoT inatoa leseni kwa watoa huduma ya malipo ambapo huzisimamia na kukagua miundombinu waliyoweka kama inafuata kanuni na misingi ya kimataifa.

Kutokana usimamizi wa mifumo hiyo kwa kufuata viwango vya kimataifa Septemba 2025 BoT ilitunukiwa Tuzo Kuu ya Ubunifu katika Huduma Jumuishi za Fedha (Nestor Espenilla Jr. Financial Inclusion Innovation Award) kutokana na utekelezaji madhubuti wa mifumo ya malipo ya kisasa, hatua inayochangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za kufanya miamala kwa wananchi na kuongeza ufanisi wa huduma za kifedha nchini.

Tuzo hiyo ilipokelewa na Naibu Gavana anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, kwa niaba ya Gavana wa Benki Kuu, Bw. Emmanuel Tutuba, mjini Swakopmund, nchini Namibia.

# KAMATI YA MIFUMO YA MALIPO: NGUZO MPYA YA UIMARA NA UFANISI WA MALIPO YA KITAIFA



Desemba 2, 2025 Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilizindua Kamati ya Mifumo ya Malipo yenye lengo la kuimarisha uratibu, utawala, na ukuzaji wa mifumo ya kitaifa ya malipo. Kamati hiyo ilizinduliwa rasmi na Naibu Gavana, Bi. Sauda Kassim Msemo, katika hafla iliyofanyika Makao Makuu Ndogo jijini Dar es Salaam.

Kuundwa kwa Kamati ya Mifumo ya Malipo ni hatua muhimu katika kuimarisha usimamizi, uratibu na maendeleo ya mifumo ya kitaifa ya malipo nchini.

Kamati hii imeanzishwa kama jukwaa la pamoja litakalowawezesha wadau wa sekta ya fedha kushirikiana kwa karibu katika kushughulikia masuala ya kimkakati yanayohusu uendeshaji na maendeleo ya mifumo ya malipo, ambayo ni mhimili muhimu wa uchumi wa kisasa.

Katika miaka ya hivi karibuni, sekta ya mifumo ya malipo imepitia mabadiliko makubwa kutokana na maendeleo ya teknolojia, ukuaji wa huduma za kifedha kidijitali, ongezeko la miamala ya fedha kwa njia ya simu (mobile money), pamoja na kuibuka kwa ubunifu wa fintech na mahitaji yanayoongezeka ya malipo ya mipakani.

Mabadiliko haya yameleta fursa kubwa za kukuza ujumuishaji wa kifedha na kuchochea shughuli za kiuchumi, lakini pia yameibua changamoto mpya katika uendeshaji wa mifumo ya malipo na usimamizi wa mifumo hiyo.

Kupitia Kamati ya Mifumo ya Malipo, Benki Kuu ya Tanzania imeunda jukwaa la pamoja la kushughulikia changamoto hizo kwa namna iliyoratibiwa na shirikishi.

Kamati hii itasaidia kuimarisha ushirikiano kati ya Benki Kuu na wadau wengine wa sekta ya malipo, kuwezesha majadiliano ya pamoja juu ya masuala ya kipaumbele, na kusaidia kufikia mwafaka katika masuala yanayohusu uendeshaji wa mifumo ya malipo na miradi ya pamoja.

Moja ya faida kuu za Kamati hii ni kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Benki Kuu katika kuweka mwelekeo wa kimkakati, malengo ya sera na uendeshaji wa jumla wa mifumo ya malipo ya kitaifa.

Ushauri huu, unaotokana na uzoefu wa vitendo wa washiriki wa Kamati, utasaidia kuhakikisha kuwa maamuzi yanayofanywa yanazingatia uhalisia wa soko na mahitaji ya wadau wote.

Aidha, Kamati itachangia katika utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza kati ya washiriki wa mifumo ya malipo, hususan katika mifumo au mipango ya malipo inayoendeshwa na Benki Kuu. Kupitia ushirikiano na majadiliano ya wazi, Kamati itasaidia kupunguza migogoro, kuimarisha uaminifu miongoni mwa wadau, na kuhakikisha uendeshaji wenye tija na utulivu wa mifumo ya malipo.

Faida nyingine muhimu ni mchango wa Kamati katika kuweka viwango na kupitia kanuni na taratibu zinazotawala mifumo ya malipo. Ushirikiano huu utawezesha mifumo ya malipo kuwa salama zaidi, yenye ufanisi, inayoweza kuunganishwa (interoperable) na inayokidhi viwango vya kimataifa, huku ikilinda maslahi ya watumiaji wa huduma za kifedha kupitia mifumo madhubuti ya ulinzi wa mlaji wa huduma za fedha.

Kwa ujumla, kuanzishwa kwa Kamati ya Mifumo ya Malipo ni hatua ya kimkakati itakayochangia kujenga mifumo ya malipo iliyo jumuishi, thabiti na endelevu. Kupitia umoja na ushirikiano wa wadau, Kamati hii inatarajiwa kuimarisha mazingira ya malipo nchini, kuchochea ubunifu, na hatimaye kuunga mkono ukuaji wa uchumi wa Taifa katika enzi ya uchumi wa kidijitali



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania anayeshughulikia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi.Sauda Msemo, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Kamati ya Mifumo ya Malipo iliyofanyika tarehe 2 Desemba 2025.



Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo wa Benki Kuu ya Tanzania, Bi. Lucy- Charles Shaidi, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Kamati ya Mifumo ya Malipo iliyofanyika tarehe 2 Desemba 2025.

# BOT YASHIRIKI MKUTANO MKUU WA 48 WA CISNA NCHINI BOTSWANA




Naibu Gavana, Bi.Sauda Msemo katika Mkutano wa CISNA unaofanyika mjini Maun, nchini Botswana kuanzia Oktoba 5 hadi 10, 2025. Kulia ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dkt. Baghayo Saqware, na Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) CPA. Nicodemus Mkama.



Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilishiriki Mkutano Mkuu wa 48 na mikutano midogo ya Kamati ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) inayohusiana na Usimamizi wa Bima, Masoko ya Fedha na Taasisi Zisizo za Kibenki (CISNA).

Mkutano huo unaofanyika mjini Maun, nchini Botswana kuanzia Oktoba 5 hadi 10, 2025, uliwakutanisha wadau kutoka nchi mbalimbali wanachama wa SADC kujadili masuala ya usimamizi na uimarishaji wa sekta zisizo za kibenki.

Ujumbe wa BoT katika mkutano huo uliongozwa na Naibu Gavana anayeshughulikia Usimamizi na Uthabiti wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo.

Benki Kuu ni mwanachama wa CISNA kutokana na jukumu lake la kusimamia uwekezaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi za fedha zisizo za kibenki, zikiwemo zinazotoa huduma ndogo za fedha. BoT ilijiunga rasmi na kamati hiyo baada ya kusaini makubaliano tarehe 6 Oktoba 2023.

Mkutano huo ulifunguliwa rasmi Jumanne, Oktoba 7, 2025, na Makamu wa Rais wa Botswana, Mhe. Ndaba Nkosinathi Gaolathe, ambaye aliipongeza CISNA kwa utendaji wake mzuri na kuhimiza kuimarishwa kwa juhudi za kuendeleza uchumi wa ukanda wa SADC.

Alisisitiza umuhimu wa wajumbe wa CISNA kubuni mikakati madhubuti ya kuinua uchumi wa wananchi wa kanda hiyo, huku akipongeza juhudi za kamati hiyo katika kukuza elimu ya kifedha na kuendeleza huduma ndogo za fedha.

CISNA ina jukumu la kuoanisha mifumo ya usimamizi wa huduma za kifedha zinazotolewa na taasisi zisizo za kibenki katika nchi wanachama wa SADC ili kuhakikisha zinazingatia viwango vya kimataifa vinavyowekwa na taasisi husika duniani.



Washiriki wa Mkutano Mkuu wa 48 na mikutano midogo ya Kamati ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) inayohusiana na Usimamizi wa Bima, Masoko ya Fedha na Taasisi Zisizo za Kibenki (CISNA).

# GAVANA TUTUBA AWATAKA WAHITIMU KUDUMISHA UADILIFU NA UZALENDO






Gavana Emmanuel Tutuba akizundua kitabu cha Mhutasari wa Tafiti za wahitimu wa Stashahada ya Uzamili katika Uongozi wa Benki. Kulia kwake ni Manaibu Gavana, Bw, Julian Banzi Raphael na Bi. Sauda Kassim Msemo, pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Mhe. Amina Makilagi.



Wahitimu. pamoja na wageni waalikwa mbalimbali katika Mahafali ya Nne ya Chuo cha Benki Kuu yaliyofanyika jijini Mwanza tarehe 28 Novemba 2025.



Gavana Emmanuel Tutuba katika picha na Menejimenti ya Chuo cha Benki Kuu pamoja na wafanyakazi baada ya Mahafali ya Nne ya Chuo cha Benki Kuu yaliyofanyika jijini Mwanza tarehe 28 Novemba 2025.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amewataka wahitimu wa Chuo cha Benki Kuu ya Tanzania kudumisha uadilifu, uzalendo na ubunifu wanapoanza safari zao katika sekta ya fedha.

Akizungumza katika Mahafali ya Nne ya Chuo hicho yaliyofanyika tarehe 28 Novemba 2025, ambako alikuwa Mgeni Rasmi, Gavana Tutuba alisisitiza kuwa sekta ya fedha ni moyo wa uchumi wa taifa hivyo inahitaji watu wenye maadili makubwa na ujuzi wa hali ya juu.

Gavana Tutuba aliwaonya wahitimu dhidi ya kushiriki vitendo visivyozingatia maadili kama wizi, udanganyifu na kusababisha mikopo chechefu, akibainisha kuwa BoT itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa wafanyakazi wa sekta ya fedha nchini na haitasita kuchukua hatua kali kwa wale watakaokiuka maadili ya kazi.

Aidha, aliwahimiza wahitimu kuwa wabunifu, wachapakazi na kutumia maarifa waliyoyapata kujiajiri au kutafuta fursa mpya katika soko la ushindani. Alisema dunia ya sasa inahitaji watu wanaoweza kuwaza nje ya mifumo ya kawaida na kutumia ujuzi wa vitendo (competency-based learning) kuleta mabadiliko chanya katika sekta mbalimbali.

Katika hotuba yake, Gavana Tutuba pia alisisitiza umuhimu wa wahitimu kuendelea kujiendeleza kitaaluma kwa kuwa mabadiliko ya teknolojia na maarifa yanakwenda kwa kasi. Alisema kuhitimu sio mwisho wa safari bali ni hatua ya kwanza ya safari ndefu ya kujifunza.

Akizungumza awali, Mkuu wa Chuo cha Benki Kuu, Dkt. Nicas Yabu, alisema kuwa Chuo hicho kinaendelea kuwa kitovu cha mafunzo ya kikanda ambapo katika mwaka 2024/25, jumla ya washiriki 127 walitoka nje ya nchi—ikiwemo Kenya, Uganda, South Sudan, Somalia, Burundi, Zambia, Zimbabwe, Comoros, Botswana na Ghana. Uwepo wa washiriki hao wa kimataifa uliingizia Benki Kuu dola za marekani 93,500, hatua inayodhihirisha ukuaji na mvuto wa programu za mafunzo zinazotolewa na chuo hicho.

Katika mahafali hayo, jumla ya wahitimu 36 walitunukiwa Stashahada ya Uendeshaji na Usimamizi wa Benki, huku wahitimu 31 wakitunukiwa Stashahada ya Uzamili katika Uongozi wa Benki.

# NAIBU GAVANA RAPHAEL AONGOZA SEMINA YA DIRA YA TAIFA



Naibu Gavana Utawala na Udhibiti wa Ndani, Julian Raphael aliongoza semina kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kuangazia mchango na nafasi ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kufikia malengo ya Dira kwa wakurugenzi na wakuu wa idara.

Semina hiyo ilifanyika Desemba 3, 2025 katika ofisi ndogo za Makao Makuu ya BoT Zanzibar ikiwa ni maandalizi kuelekea Mkutano wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa BoT lililofanyika Desemba 4 hadi 6, 2025.

Akiongoza semina hiyo, Naibu Gavana Raphael alisisitiza kwa viongozi hao kuhakikisha mipango inayowekwa katika kurugenzi na idara zao zinalenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Aidha, wajumbe hao walipatiwa mafunzo ya namna sahihi ya kutumia akili mnemba na jinsi jinsi akili mnemba inavyoweza kuinua tija katika utendaji wa wafanyakazi wa Benki Kuu.

Kwa upande wao, wajumbe wa semina hiyo walishukuru na kuomba wafanyakazi wajengewe uwezo zaidi katika maeneo hayo kwa ajili ya kuendelea kuinua utendaji wao.

**Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (Utawala na Udhibiti wa Ndani), Bw. Julian Raphael, akizungumza katika semina ya iliyoangazia mchango wa Benki Kuu katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa BoT. semina hiyo ilifanyika tarehe. Semina hiyo ilifanyika Desemba 3, 2025 katika ofisi za BoT Zanzibar.**



# BOT YAKUTANA NA WADAU KUJADILI MPANGO MKAKATI WAKE WA MIAKA MITANO





Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imekutana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kufanya tathmini ya Mpango Mkakati wake wa miaka mitano (2021/22–2025/26) pamoja na kukusanya maoni yatakayosaidia katika kuandaa Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano ijayo, unaoanzia mwaka 2026/27 hadi 2030/31.

Wadau walioshiriki katika kikao hicho kilichofanyika tarehe 12 Desemba 2025, ni pamoja na viongozi na wawakilishi kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi zake, wawakilishi kutoka taasisi za kitaaluma, pamoja na wakuu wa mabenki na taasisi za fedha nchini.

Akizungumza katika kikao hicho, Naibu Gavana wa Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, alisema kuwa Benki Kuu inaona umuhimu mkubwa wa kukutana na wadau wake ili kujadiliana masuala mbalimbali na kupokea maoni yao kwa lengo la kustawisha uchumi wa nchi.

“Hapo zamani, benki kuu ulimwenguni kote zilikuwa zikijifungia ndani, zilikuwa hazitoki hadharani kuzungumza na wadau wake. Lakini katika karne hii ya 21, kunahitajika uwazi, ni lazima benki kuu zishirikishe wadau wake kabla ya kupanga mikakati mbalimbali inayolenga kustawisha uchumi wa nchi husika”, alisema Dkt. Kayandabila.

Aliongeza kuwa kwa kuzingatia umuhimu huo, Benki Kuu ya Tanzania iliandaa kikao hicho ili kufanya tathmini ya Mpango Mkakati uliopo na kupokea maoni ya wadau kwa ajili ya kuboresha mpango mkakati ujao.

"Katika kikao kazi hichi tutaangalia safari yetu ya miaka mitano, yaani nini tumefanya katika kipindi cha miaka mitano na wapi tunaelekea", alieleza Naibu Gavana huyo.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kupitia usimamizi mzuri wa Benki Kuu, Tanzania imeendelea kubaki katika orodha ya nchi zenye uchumi wa kati wa chini (lower-middle-income). Hali hii imetokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, ushauri wa kiuchumi na kibajeti unaotolewa na Benki Kuu kwa serikali zote mbili pamoja na uimarishaji wa utafiti unaosaidia katika kutunga sera ya fedha yenye ubora na kutoa ushauri wa uchumijumla.

Aidha, katika kipindi hicho sekta ya kibenki imeendelea kuwa tulivu na yenye ukwasi wa kutosha, kufuatia kuongezeka kwa imani ya umma katika huduma na mifumo ya kibenki nchini.

Naye, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA) ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Bw. Theobald Sabi, aliipongeza BoT kwa kuendeleza utaratibu huo wa kukusanya maoni ya wadau yanayosaidia katika kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano wa Benki Kuu. Alisema kuwa hatua hiyo shirikishi ina mchango mkubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi.



Naibu Gavana Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika kikao cha BoT na wadau mbalimbali kilichofanyika tathmini ya Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Benki Kuu (2021/22–2025/26) na kukusanya maoni kwa ajili ya mpango mkakati ujao, kilichofanyika tarehe 12 Desemba 2025 katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

# GAVANA BOT AIWAKILISHA TANZANIA UAPISHO RAIS MPYA WA AFREXIMBANK



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, aliiwakilisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hafla ya kumuaga Rais wa tatu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Uuzaji na Uagizaji Nje ya Afrika (Afreximbank), Prof. Benedict Oramah, na kumkaribisha Rais mpya, Dkt. George Elombi.

Dkt. Elombi anakuwa Rais wa Nne wa Afreximbank akiwa amehudumu katika taasisi hiyo tangu mwaka 1996. Dkt. Elombi ambaye aliapishwa tarehe 25 Oktoba 2025 alimpongeza mtangulizi wake Prof. Oramah na ameahidi kudumisha mafanikio ya Afreximbank katika kustawisha sekta ya fedha barani Afrika na uchumi kiujumla.

Hafla hiyo iliyofanyika tarehe 24 na 25 Oktoba 2025 jijini Cairo, Misri, iliwakutanisha viongozi wa sekta ya fedha, wakuu wa mabenki, wawakilishi wa serikali, na wadau wa maendeleo kutoka ndani na nje ya bara la Afrika,.

Viongozi hao walimpongeza Prof. Oramah kwa kuimarisha ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi wanachama wa Afrika kupitia programu na mikakati ya ubunifu iliyotekelezwa na benki hiyo pamoja na juhudi za kukuza biashara ya ndani ya bara la Afrika na kupunguza utegemezi wa masoko ya nje.




Waziri wa Fedha na Waziri Mshirikishaji wa Uchumi wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (kulia), Mhe. Wale Edun, akitoa hotuba kabla ya kumtambulisha rasmi Rais mpya wa Benki ya Afreximbank Dkt George Elombi aliyesimama kushoto.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Oramah alitoa shukrani kwa viongozi mbalimbali wa bara la Afrika kwa ushirikiano wao na kusisitiza umuhimu wa kuwekeza katika rasilimali watu, ubunifu wa kiteknolojia, na utafiti wa kiuchumi ili kujenga Afrika yenye kujitegemea kifedha.

Aidha, kupitia Afreximbank, Tanzania inategemea kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwemo kujenga kituo cha umahiri cha afya hapa nchini (African Medical Centre of Excellence).

Afreximbank, yenye nchi zaidi ya 50 wanachama, ilianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kukuza biashara ya ndani na nje ya Afrika. Kupitia miradi kama Intra-African Trade Initiative, Project Preparation Facility, na Pan-African Payment and Settlement System (PAPSS), Benki hii imechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya viwanda, miundombinu, na biashara barani Afrika.



Dkt. George Elombi (kulia) akisaini hati rasmi ya kiapo cha uwakilishi wa mamlaka katika hafla iliyoongozwa na Waziri wa Fedha na Waziri Mshirikishaji wa Uchumi wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria, Bw. Wale Edun (katikati).

# BOT DODOMA YAKABIDHI JENGO LA JIKO KITUO CHA WATOTO YATIMA

Tawi la Benki Kuu Dodoma limekabidhi rasmi jengo la jiko la kisasa lenye thamani ya TZS 17 milioni kwa kituo cha watoto yatima cha Qadiriya kilichopo eneo la Ndachi, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wake wa Kurudisha kwa Jamii (CSR).
Makabidhiano ya jengo hilo yalifanyika, Oktoba 17, 2025, yakiongozwa na Meneja wa Idara ya Fedha na Utawala wa BoT Tawi la Dodoma, Dkt. Francis Assenga.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dkt. Assenga alisema Benki Kuu itaendelea kushirikiana na jamii inayoizunguka kwa kutoa misaada ya hali na mali pale inapowezekana. Alipongeza pia uongozi wa kituo hicho kwa kazi nzuri ya kuwalea watoto katika misingi ya maadili mema na upendo.

"Benki Kuu itaendelea kuwa karibu na jamii kwa kushiriki katika miradi yenye manufaa kwa wananchi. Tunawapongeza wasimamizi wa kituo hiki kwa kujitolea katika malezi bora ya watoto hawa," alisema Dkt. Assenga.

Kwa upande wake, Msimamizi wa Kituo cha Qadiriya, Sheikh Said Kulele, aliishukuru Benki Kuu kwa msaada huo, akisema kuwa jiko hilo jipya litaboresha kwa kiwango kikubwa mazingira ya maandalizi ya chakula kwa watoto.

"Tunaishukuru sana Benki Kuu kwa kujitoa katika hili, jiko hili limetusaidia kutoka kupika katika kibanda kidogo na duni na sasa hivi tutaandaa chakula katika mazingira rafiki zaidi kwa watoto wetu. Tunaomba muendelee kutushika mkono katika kuboresha mazingira ya watoto hawa,"amesema Sheikh Kulele.
Awali, Meneja Msaidizi wa Rasilimali Watu na Utawala, Tawi la BoT Dodoma, Bw. Airenus Mlowe, alieleza kuwa wazo la kutoa msaada huo lilitokana na ziara ya Benki hiyo katika kituo hicho wakati wa hafla ya Iftari ya pamoja, ambapo walibaini changamoto kubwa katika eneo la upishi.

Ujenzi wa jiko hilo unatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kuboresha ustawi na huduma kwa watoto wanaolelewa katika kituo hicho.



Meneja wa Idara ya Fedha na Utawala, Tawi la BoT Dodoma, Dkt. Francis Assenga (kulia) akimkabidhi Msimamizi wa Kituo cha Qadiriya, Sheikh Said Kulele, jengo la jiko la kisasa kwa kituo cha watoto yatima cha Qadiriya kilichopo Dodoma.



Watoto wanaolelewa katika kituo cha Qadiriya wakifanya dua baada ya kukabidhiwa jengo la jiko la kisasa tarehe 17 Oktoba 2025.



Jiko lililotumiwa na Kituo cha Qadiriya kabla ya kujengewa jiko la kisasa na Tawi la BoT Dodoma.

# WATAALAMU BENKI KUU SHELISHELI WAPIGWA MSASA KUHUSU MIFUMO YA TEHAMA YA BOT, WAVUTIWA NA MAKUMBUSHO YAKE




Wataalamu mbalimbali kutoka Benki Kuu ya Shelisheli (CBS) walitembelea Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa ajili ya kujifunza jinsi BoT inavyotengeneza na kuendesha mifumo yake ya TEHAMA kwa kutumia wataalamu wa ndani ya taasisi.

Ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 10 hadi 14 Novemba 2025 katika ofisi za BoT Jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, wataalamu hao walipatiwa muhtasari wa namna BoT inavyotengeneza na kuendesha mifumo yake, taratibu za uhakiki wa ubora, pamoja na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha usalama wa mifumo hiyo.

Aidha, walielimishwa kuhusu mchakato uliotumika katika utengenezaji wa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Hapo (TIPS) pamoja na Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (iCBS), yote ikiwa ni mifumo iliyotengenezwa na wataalamu wa ndani ya taaisisi.

Pia, wataalamu hao kutoka Shelisheli walipata fursa ya kutembelea Makumbusho ya Benki Kuu ya Tanzania, ambapo walielezwa kuhusu historia ya fedha nchini, pamoja na historia ya BoT tangu kuanzishwa kwake tarehe 14 Juni 1966.

Akizungumza baada ya kutembelea makumbusho hayo, mmoja wa wataalamu kutoka CBS aliipongeza Benki Kuu ya Tanzania kwa kuanzisha makumbusho yake yenye maudhui ya kina yanayoelezea historia ya maendeleo ya uchumi na sekta ya fedha nchini kwa muktadha wa tulipotoka, tulipo na tunapoelekea.

Ikumbukwe kwamba Julai 30 2025, akizingumza katika hafla ya uzinduzi wa iCBS, Makamu wa Rais Mstaafu, Dkt. Philip Mpango, aliitaja Benki Kuu ya Tanzania kama mfano wa kuigwa kwa namna inavyotumia wataalamu wake wa ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali jambo linalosaidia kukamilika kwa wakati na kwa ubora stahiki.




Afisa Uhusiano wa Umma wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Daniel Mlimuka, akitoa maelezo kwa wataalamu kutoka Benki Kuu ya Shelisheli, kuhusu historia ya fedha na historia ya Benki Kuu.



# BENKI KUU YA RWANDA YAFANYA ZIARA YA MAFUNZO BOT



Katika kuhakikisha Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inakuwa kitovu cha maarifa na uga wa kujifunza ilitembelewa na wataalamu kutoka Benki Kuu ya Rwanda (BNR).

Wataalamu hao walitembelea BoT kwa ajili ya kujifunza jinsi inavyotengeneza na kuendesha mifumo ya TEHAMA kwa kutumia wataalamu wa ndani ya taasisi na kubadilishana uzoefu.

Katika ziara hiyo iliyofanyika kuanzia Novemba 24 hadi 27, 2025 katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam, wataalamu hao walijifunza kuhusu mbinu bora zilizosaidia Benki Kuu ya Tanzania kufanikisha matumizi ya mifumo ya kidijitali, pamoja na mikakati ya kuimarisha ufanisi wa mifumo ya usimamizi wa nyaraka katika taasisi za kifedha,

Aidha walijifunza namna BoT inavyotengeneza na kuendesha mifumo yake, taratibu za uhakiki wa ubora, pamoja na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha usalama wa mifumo hiyo.

Wataalamu hao kutoka Rwanda walipata fursa ya kutembelea makumbusho ya Benki Kuu ya Tanzania, ambapo walielezwa kuhusu historia ya fedha nchini, pamoja na historia ya BoT tangu kuanzishwa kwake Juni 14, 1966.

Vilevile, walieleza kuridhishwa kwao na maarifa waliyopata, wakisema kuwa uzoefu huo utasaidia kwa kiasi kikubwa katika maboresho ya mifumo yao.

Ziara hiyo ilihitimishwa kwa pande zote mbili kuahidi kuendelea kushirikiana katika masuala ya teknolojia na mifumo, ikiwa ni hatua muhimu ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika sekta ya fedha.



Wataalamu kutoka Benki Kuu ya Rwanda (Kushoto) wakijifunza namna mifumo ya kidijitali ya BoT inavyofanya kazi.





Wataalamu kutoka kutoka Benki Kuu ya Rwanda na Benki Kuu ya Tanzania wakijifunza historia ya fedha na huduma za kibenki nchini Tanzania, walipotembelea makumbusho ya Benki Kuu ya Tanzania. Anayewaelekeza ni Afisa kutoka Idara ya Mawasiliano Benki Kuu ya Tanzania, Bi Catherine Nyoni.

# BENKI KUU YA TANZANIA

## SALAMU ZA PONGEZI



**MHE. BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI**
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**MHE. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI**
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Benki Kuu ya Tanzania inatoa pongezi kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Makamu wa Rais, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi.

Pia, inatoa pongezi kwa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Pili katika awamu ya Nane.

Benki Kuu itaendelea kuhudumia Serikali zote mbili katika kuandaa na kusimamia sera madhubuti za uchumi ili kuchochea maendeleo endelevu na ustawi wa Taifa kwa ujumla.

# MAREKANI KUTEKELEZA MIRADI MIKUBWA YA UWEKEZAJI NCHINI, RAIS SAMIA ATOA NENO





Tanzania ipo mbioni kunufaika na uwekezaji mkubwa kutoka Marekani, baada ya nchi hizo mbili kukubaliana kuharakisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati inayolenga kukuza uchumi, kufungua ajira na kuimarisha ushirikiano wa muda mrefu wa kiuchumi.

Hayo yalijadiliwa Desemba 8, 2025 katika mazungumzo kati ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Mhe. Andrew Lentz, yaliyofanyika Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma.

Katika majadiliano hayo pande zote zilikubaliana kukamilisha hatua za mwisho kabla ya kutia saini mikataba rasmi.

Katika taarifa iliyotolewa na Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Bw. Shaaban Kissu ilisema; "Miongoni mwa miradi mikubwa inayotarajiwa kutekelezwa ni mradi wa Gesi Asilia (LNG) wenye thamani inayokadiriwa kufikia USD bilioni 42, unaohusisha kampuni za kimataifa za nishati.

"Mradi huo unatarajiwa kuchochea matumizi ya rasilimali gesi iliyopo baharini, kuongeza mapato ya taifa, kuzalisha maelfu ya ajira na kuiweka Tanzania kwenye ramani ya wazalishaji wakubwa wa LNG duniani."

Taarifa hiyo iliongeza kuwa mradi mwingine ni ule wa Tembo Nickel uliopo Ngara mkoani Kagera, wenye thamani ya takribani USD milioni 942, unaolenga uchimbaji wa madini ya nikeli yanayotumika kwa kiwango kikubwa katika utengenezaji wa betri za magari ya umeme.

"Mradi huu unatazamiwa kuongeza mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa taifa na kuimarisha nafasi ya Tanzania kwenye soko la nishati safi duniani,"ilieleza taarifa hiyo

Aidha, Tanzania inatarajia kuanza utekelezaji wa Mradi wa Mahenge Graphite wenye thamani ya USD milioni 300, ambao ni miongoni mwa miradi mikubwa zaidi ya uzalishaji wa grafiti yenye ubora wa kiwango cha juu duniani. Mradi huo unalenga kukidhi mahitaji ya grafiti katika sekta ya nishati jadidifu na teknolojia za kisasa, huku ukiiweka Tanzania kama mzalishaji muhimu wa madini hayo kimataifa.

Akizungumza katika mazungumzo hayo, Rais Samia alisisitiza kuwa miradi hiyo ni ya kimkakati kwa taifa, ikilenga kuimarisha uwekezaji, kuongeza ajira na kuinua ustawi wa wananchi, huku Tanzania ikiendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kufuata taratibu zilizo wazi na rafiki kwa wawekezaji.

Pia, Rais Samia alisisitiza kuwa Tanzania haifungamani na upande wowote hivyo ipo tayari kushirikiana na nchi yoyote wanaoheshimu uhuru wa Tanzania.

"Kama taifa lisilofungamana na upande wowote, Tanzania iko wazi na tayari kushirikiana na washirika wote wanaoheshimu uhuru na kuthamini maono yetu ya ustawi," alisema Rais Samia

Kwa upande wake, Kaimu Balozi Lentz alisema zaidi ya kampuni 400 za Marekani tayari zinafanya kazi nchini, akisisitiza dhamira ya Marekani kuendelea kuunga mkono utekelezaji wa miradi mikubwa inayochochea maendeleo ya kiuchumi na ushirikiano wa pande mbili.

Makubaliano hayo yanaashiria mwanzo mpya wa ushirikiano wa uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani, yakitarajiwa kufungua ukurasa mpya wa maendeleo unaoendeshwa na sekta binafsi, kuhimiza uhamishaji wa teknolojia na kuimarisha mahusiano ya kiuchumi ya muda mrefu kati ya mataifa hayo mawili.

# RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN APOKEA TUZO TATU ZA UTALII ZA TANZANIA




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Tuzo ambayo Tanzania imeshinda kuwa eneo bora la Utalii wa Safari Duniani (World's Leading Safari Destination) kutoka kwa Waziri wa Maliasili na Utalii Dkt. Ashatu Kijaji, Ikulu ndogo ya Tunguu Zanzibar tarehe 05 Januari, 2026. Tuzo hiyo imetolewa na Taasisi ya World Travel Awards (WTA) yenye Makao Makuu yake Jijini London, Uingereza.




Muonekano wa Tuzo tatu za "WORLD TRAVEL AWARDS" ambazo Tanzania imeshinda.






# BALOZI DKT. NCHIMBI ASHIRIKI AU-EU SUMMIT, UCHUMI WAGUSIWA

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ameshiriki Mkutano wa saba wa viongozi wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Ulaya (AU-EU Summit).

Mkutano huo wa siku mbili ulifanyika Jijini Luanda nchini Angola Novemba 25, 2025.

Pamoja na mambo mengine umehitimishwa kwa dhamira ya kuunda mustakabali mwema na endelevu wa Afrika na Ulaya, ushirikiano mpya na imara juu ya amani, usalama na utawala katika kukabiliana na vita na migogoro ulimwenguni.

Masuala mengine yaliyopewa kipaumbele katika Mkutano huo ni pamoja na ahadi madhubuti ya ushirikiano wa kimataifa pamoja na ushirikiano imara na wa kuheshimiana katika masuala ya uhamiaji na uhamaji.

Mkutano huo pia umedhamiria kuendelea kusaidia nchi zote za Kiafrika katika maendeleo, viwanda, kuongeza mauzo ya nje, na kuunganisha katika masoko ya kikanda. Pia makubaliano yamefanyika katika nia ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA).

Pia kukuza maendeleo endelevu kwa kuzingatia minyororo ya thamani kwa kuongeza uwezo wa viwanda vya ndani kushiriki katika masoko ya kikanda na kimataifa, ikiwemo uongezaji thamani wa madini adimu.

Ili kuwezesha biashara, Mkutano huo, umesisitiza umuhimu wa kudumisha uwazi, na njia zinazojumuisha mazungumzo, ikijumuisha biashara na shughuli za kimazingira, na kukuza ushirikiano kupitia kujenga uwezo na usaidizi wa kiufundi ili kusaidia nchi za Kiafrika kuondoa kaboni na kusimamia rasilimali asilia kwa njia endelevu.

Mkutano huo umedhamiria kushughulikia mabadiliko ya tabianchi na kukuza uendelevu wa mazingira, kwa kutatua changamoto pamoja zinazoletwa kwa wauzaji bidhaa kutoka Afrika kwa njia endelevu.
Pia, mkutano huo umeadhimisha miaka 25 ya ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya na Umoja wa Afrika.

Mkutano huo umefanyika chini ya kauli mbiu isemayo "Kukuza amani na ushirikiano kupitia Ustawi wa Kimataifa wenye Tija" (promoting peace and prosperity through effective Multilateralism)

# WAZIRI MKUU AWAPA MAAGIZO TANROADS, TARURA




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Nchemba, amewaagiza Watendaji Wakuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kufanya tathmini ya kina ya miradi yote ya ujenzi wa barabara iliyokwisha lipwa fedha za awali, ili kubaini hatua halisi za utekelezaji na thamani ya kazi iliyofanyika.

Agizo hilo lilitolewa Desemba 17, 2025, wakati Waziri Mkuu akizungumza na wananchi baada ya kukagua uharibifu wa miundombinu mbalimbali uliofanyika Oktoba 29, 2025 katika ziara yake ya kikazi mkoani Songwe.

Dkt. Mwigulu alisema tathmini hiyo inalenga kuhakikisha utekelezaji wa miradi unaendana na kiasi cha fedha kilichokwisha kutolewa kwa wakandarasi, akisisitiza kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika kufanya kazi chini ya kiwango.

“Na ikiwa itapatikana miradi ambayo imefanyika chini ya kiwango cha fedha iliyopatikana, hiyo ni hujuma dhidi ya uchumi wa nchi yetu, na wahusika lazima wafikishwe kwenye mkono wa sheria,” amesema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amekemea tabia ya baadhi ya wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kwa ufanisi licha ya kulipwa fedha, huku akielekeza kuwa mkandarasi aliyeshindwa kutimiza wajibu wake katika mradi wa Mbinga asipewe kazi nyingine yoyote nchini.

“Haiwezekani tumpatie mtu fedha halafu aje atuchezee hapa. Wale wote mnaowalipa fedha halafu wanazitumia kulipa madeni yao, huku hawawalipi wazawa waliowapatia huduma, wasipate kazi tena,” alisisitiza.

Aidha, Waziri Mkuu amewaagiza TANROADS na TARURA kuhakikisha mikataba yote ya ujenzi wa miradi ina kipengele kinachowalazimisha wakandarasi kufungua akaunti za malipo ndani ya Tanzania, ili kuzuia fedha za miradi kutumwa nje ya nchi na kuchelewesha utekelezaji.

“Haiwezekani mradi unafanyika Tanzania, halafu fedha zake zilipwe kwenye akaunti za nchi nyingine. Zikifika kule wanalipa madeni yao, huku miradi ikisimama. Hakikisheni kwenye mikataba kuna kipengele cha kufungua akaunti hapa hapa nchini,” amesema.

Agizo la Waziri Mkuu linakuja katika kipindi ambacho Serikali inaendelea kuwekeza fedha nyingi kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara kupitia TANROADS na TARURA, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuchochea uchumi, kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na huduma, pamoja na kuboresha maisha ya wananchi hususan vijijini.

Akihitimisha ziara hiyo, Dkt. Mwigulu aliwataka viongozi wote nchini kutokaa ofisini pekee bali kuwafikia wananchi kwenye maeneo yao, kusikiliza changamoto zao na kushirikiana nao katika kuzitatua kwa vitendo.

# RAIS MWINYI ATAJA UMUHIMU WA UKUSANYAJI MAPATO KATIKA UCHUMI





Kwa kutambua umuhimu wa ukusanyi wa mapato wenye ufanisi katika uchumi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika juhudi za kuimarisha utendaji wa taasisi hiyo.

Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo Desemba 17, 2025, alipokutana na Kamishna Mkuu wa TRA, Bw. Yussuf Juma Mwenda, pamoja na baadhi ya watendaji wakuu wa Mamlaka hiyo, waliofika Ikulu, Zanzibar, kwa lengo la kujadili masuala ya ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma.

Amesema mapato ni mhimili mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na kuitaka TRA kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma katika kila eneo lenye fursa ya kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

Rais Dkt. Mwinyi ameongeza kuwa; "Hatua hiyo ni muhimu kutokana na ukuaji wa kasi wa shughuli za bandari Zanzibar, kama vile Bandari ya Fumba kwa sasa ni miongoni mwa bandari zinazokua kwa kasi kufuatia ongezeko la usafirishaji wa mizigo."

Aidha, amebainisha kuwa Serikali imeweka mikakati maalum kwa bandari za Pemba kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo, hatua itakayowaletea unafuu wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dkt. Mwinyi amepongeza hatua inayochukuliwa na TRA ya kuweka Scanner mpya bandarini, akibainisha kuwa hatua hiyo itaongeza mapato ya Serikali na kuimarisha usalama wa nchi.

Kwa upande wake, Kamishna Mkuu wa TRA, Bw. Mwenda, ameonesha kufarijika na ushirikiano unaoendelea kupatikana kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hali inayochangia kuimarisha utoaji wa huduma za Mamlaka hiyo kwa ufanisi.

Aidha, Kamishna Mkuu huyo amefahamisha kuwa TRA inaendelea na mpango wa kuweka Scanner katika bandari zote nchini kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na udhibiti wa mapato ya Serikali.



# WIZARA YA FEDHA YAPATA WAZIRI, MANAIBU WAZIRI WAPYA



'Wabobezi, wenye uzoefu, wachapakazi na waadilifu' Sifa hizi zinatosha kuwaelezea Waziri na Manaibu Waziri wapya walioteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongoza Wizara ya Fedha.

Viongozi hao waliapishwa rasmi Novemba 18, 2025 huku Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar akiwa mkuu mpya wa wizara hiyo akirithi mikoba ya Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye aliteuliwa na kupitishwa kuwa Waziri Mkuu.

Balozi Omar, anasaidiwa na manaibu wawili ambao ni Mhe. Laurent Deogratius Luswetula pamoja na Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde.

**Alichokisema Waziri Balozi Omar**

Akizungumza na menejimenti na wafanyakazi wa wizara hiyo kwa mara ya kwanza tangu aapishwe, Mhe. Balozi Omar alisema wizara hiyo imebeba matumaini ya Serikali na Wananchi katika kuhakikisha inatafuta fedha za kuendeleza ujenzi wa miradi ya maendeleo itakayochochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi.

"Wizara inatakiwa kuweka mikakati na mipango madhubuti ya kutafuta rasilimali za ndani kwa ajili ya kuendeleza na kukamilisha miradi mbalimbali pamoja na kuweka sera bora za fedha zitakazosaidia kuyawezesha makundi mbalimbali wakiwemo ya vijana kupata ajira na kufanya biashara,"alisema Mhe. Balozi Omar

Alisema kuwa Wizara ya Fedha ndio moyo wa Serikali kwa maendeleo ya nchi hivyo Menejimenti na Wafanyakazi wote wanapashwa kujipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana lakini pia kwa kuyasikiliza makundi mbalimbali yenye changamoto zinazokwaza ustawi wao wakati nchi ikianza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Kwa upande wao, Naibu Mawaziri wa Fedha, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb), na Mhe. Laurent Deogratius Luswatula, wameshukuru kwa mapokezi makubwa waliyoyapata kutoka kwa Menejimenti na Wafanyakazi wa Wizara na kuahidi kutoa ushirikiano na kuwa chachu ya mafanikio ya kuwaletea wananchi maendeleo kama walivyoaminiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Nyadhifa alizowahi kushika Mhe. Balozi Omar

Kabla hajateuliwa kuwa Waziri wa Fedha, Balozi Omar alikuwa Balozi wa Tanzania nchini China kuanzia mwaka 2023 hadi 2025.

Pia, aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kabla ya kushika nyadhifa hizo kubwa, alipata uzoefu mkubwa katika usimamizi wa kodi, akipanda kutoka cheo cha mtoza ushuru katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuwa Naibu Kamishna wake wa shughuli za Zanzibar kati ya mwaka 1986 na 2002.

Uzoefu wake wa kifedha umechangiwa na utumishi wa awali kwenye bodi za taasisi mbalimbali kama vile Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRA), pia amewahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tanga Cement mwaka 2005.




Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) (Katikati), akimkabidhi Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Bw. Hamis Livembe, tuzo ya kupongeza wafanyabiashara katika kusaidia kuvunja rekodi ya ukusanyaji mapato kwa nusu mwaka wa fedha 2025/26, wakati wa Mkutano wa Kutathmini Utendaji Kazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa Nusu Mwaka wa Fedha 2025/26 (Mid-Year Performance Review Meeting), uliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), jijini Arusha.

# WAZIRI WA FEDHA AIPONGEZA TRA KWA UTENDAJI MZURI WA MAKUSANYO YA MAPATO

Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar (MB), ameipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hatua iliyochangia kuimarika kwa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini.

Ametoa Pongezi hizo wakati akifungua Mkutano wa Kutathmini Utendaji Kazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa Nusu Mwaka wa Fedha 2025/26 (Mid-Year Performance Review Meeting), uliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), jijini Arusha.

Mhe. Balozi Khamis, alisema kuwa Mamlaka hiyo imeendelea kuonesha ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ambapo katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025 ilikusanya shilingi trilioni 18.77 sawa na ufanisi wa asilimia 103.7 ya lengo la kukusanya trilioni 18.10.

“Mwezi Desemba pekee, TRA mmeweka rekodi mpya kwa kukusanya shilingi trilioni 4.13 kiwango cha juu zaidi kuwahi kufikiwa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hii, mafanikio haya ni kiashiria tosha kwamba TRA ipo katika mwelekeo mzuri wa kufanikisha na hata kuvuka lengo la mapato lililopangwa kwa mwaka wa fedha 2025/26. Hongereni sana kwa jitihada zenu,” alisema Mhe. Balozi Khamis.

Aidha, aliongeza kuwa mafanikio hayo yanatokana na sera na miongozo madhubuti inayowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa uwekezaji wa mifumo ambao umeleta mapinduzi katika makusanyo ya kodi.

“Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha uchumi kupitia mageuzi ya mifumo ya mapato, sera bora za kodi na matumizi ya teknolojia za kisasa katika ukusanyaji wa mapato na yameiwezesha TRA kufanya vizuri zaidi mwaka hadi mwaka,” alisema Mhe. Balozi Khamis.

Mhe. Balozi Khamis, aliitaka TRA kuhakikisha Mfumo Mpya wa IDRAS unafanya kazi kwa ufanisi mara tu baada ya kuzinduliwa rasmi, ili kuongeza uwazi, ufanisi na usimamizi bora wa ukusanyaji wa mapato sambamba na kuendelea kupanua wigo wa kodi, hasa katika sekta isiyo rasmi, biashara mtandaoni na uchumi wa kidijitali, pamoja na kutumia mbinu rafiki na zenye kuzingatia utu wa mlipakodi ili kujenga uhusiano wa kuaminiana kati ya TRA na walipakodi.

Kwa upande wao Naibu Mawaziri wa Fedha, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb) na Mhe. Laurent Luswetula, wameahidi kutoa ushirikiano kwa Mhe. Waziri wa Fedha, ili kuhakikisha wanaisimamia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili iweze kuendelea kutimiza malengo yake ya muda mfupi na mrefu ya kukusanya mapato, na kuboresha zaidi uhusiano wake na walipa kodi.

Akizungumza kwa Niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dkt. Albina Chuwa, alisema kuwa wataendelea kuhakikisha wanapanua zaidi wigo wa walipa kodi kutoka milioni 7 waliopo hivi sasa hadi milioni 21 ili kuwa na mapato mengi zaidi kusaidia ujenzi wa miradi ya wananchi.

Kwa upande wake Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bw. Yusuph Mwenda, aliwapongeza wafanyabiashara kwa namna walivyotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari na kuwezesha kufikia malengo waliyofikia katika Nusu Mwaka wa Fedha 2025/26.

Bw. Mwenda alisema kuwa kupitia Mkutano huo TRA itatathmini miezi sita ijayo, maeneo ya kuboresha zaidi ili kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ifikapo Juni 2026 baada ya TRA imeweza kurekodi Ukuaji chanya wa asilimia 13.6 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, hali inayoonesha matokeo chanya kwa Mamlaka kusimamia mapato ya Serikali, pamoja na juhudi za Serikali kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini.

“Ufanisi wa makusanyo uliofikiwa na TRA kwa miezi ya Julai hadi Desemba 2025 ni kiashiria chanya katika kuhakikisha kuwa lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/26 la Shilingi trilioni 36.06 linafikiwa” aliongeza Bw. Mwenda

Aliongeza kuwa Mamlaka hiyo imeweka lengo la kuhakikisha sehemu ya makusanyo ya mapato kwenye Pato la Taifa (revenue to GDP ratio) kwa mwaka 2025/26 inakuwa ni zaidi ya asilimia 14.1, toka kwenye kiwango cha asilimia 13.7 kilichorekodiwa mwaka 2024/25 ambapo katika kufanikisha hilo, Menejimenti ya TRA imeendelea kutekeleza kikamilifu mikakati iliyojiwekea, ikiwemo kuhakikisha kuwa Mfumo wa Usimamizi wa Kodi za Ndani Uliohuishwa (IDRAS) unaanza kutumika kuanzia Mwaka huu 2026.



# PROF MKUMBO: MABORESHO MAZINGIRA YA BIASHARA YATAONDOA VIKWAZO VYA UWEKEZAJI




Serikali imesema maboresho ya mazingira ya biashara na uwekezaji nchini yataondoa vikwazo vinavyokwamisha wawekezaji na kuongeza ushindani wa Tanzania katika kuvutia mitaji ya ndani na nje, hatua inayotarajiwa kuchochea mapinduzi makubwa ya kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, Novemba 28, 2025 jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (TISEZA) pamoja na Bodi ya Mwongozo wa Watoa Huduma kwa Wawekezaji (ISPs).

Profesa Mkumbo alisema; "Serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI II), ambao utaweka msingi wa kuondoa vikwazo vya kufanya biashara na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji, sambamba na kuongeza ushindani wa Taifa katika kuvutia wawekezaji."

Alieleza kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inatambua wazi kuwa uchumi imara na endelevu hauwezi kupatikana bila kuwepo kwa mazingira rafiki ya biashara na uwekezaji, yanayojengwa juu ya taasisi imara, utawala wa sheria, utulivu wa kisiasa na sera thabiti za kiuchumi.

Katika hatua nyingine, Profesa Mkumbo aliagiza TISEZA kuhakikisha inavutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 15 na kusajili angalau miradi 1,500 katika skimu zote za uwekezaji nchini, lengo ambalo alisema litasaidia kuongeza ajira, mapato ya Taifa na kasi ya ukuaji wa uchumi.

Akitaja vigezo vinavyochochea uwekezaji, alisema ni pamoja na ukubwa wa soko, upatikanaji wa mitaji, pamoja na fursa zilizopo katika sekta za kilimo, viwanda, madini na nishati.
Aidha, alibainisha kuwa Dira ya 2050 imeweka msisitizo mkubwa katika kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kutumia vyema nafasi ya kijiografia ya Tanzania kama lango la kibiashara kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kuhusu mikakati ya kuongeza ushiriki wa vijana katika uwekezaji, Profesa Mkumbo alisema Serikali itaanzisha kituo maalumu cha kuhudumia wawekezaji vijana, kuanzisha programu ya kuwawezesha vijana kuanzisha viwanda, kusogeza huduma za TISEZA katika kila mkoa ifikapo mwaka 2028, pamoja na kubuni vivutio vipya vya uwekezaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TISEZA, Gilead Teri, alisema mamlaka hiyo itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kutumia ubunifu na mifumo ya kisasa, huku ikipewa kipaumbele maalumu kwa wawekezaji vijana kwa kutenga maeneo mahsusi na kuwasaidia kuanzisha miradi yenye tija na inayozalisha ajira.

Hatua hizo, kwa mujibu wa Serikali, zinatarajiwa kuimarisha mazingira ya biashara, kuondoa vikwazo vya uwekezaji na kuifanya Tanzania kuwa kituo kinachovutia uwekezaji endelevu ndani na nje ya nchi.

# MAFANIKIO YA TIRA MIAKA MINNE YA MHE. RAIS SAMIA SULUHU HASSAN



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inapozungumzia miaka minne ya uwepo wa madarakani wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inazungumzia mabadiliko makubwa katika sekta ya bima, huku kukiwa na maeneo kadhaa yaliyoongezwa katika ukataji bima, hivyo kufanya maisha ya Watanzania wengi kuwa ya uhakika.

Ni wazi kuwa Miaka Minne ya Dkt Samia, Sekta ya Bima imekuwa na utekelezaji mzuri wa Sera na imeendelea kuimarika kwani Serikali imeweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara katika sekta mbalimbali nchini ikiwemo sekta ya bima nchini.

Kwa sasa Watanzania wengi zaidi wananufaika na huduma za bima, huku fidia zikitolewa kwa walioathirika na majanga mbalimbali, hivyo kusaidia kulinda maisha na mali zao.

Mafanikio haya yametokana na juhudi mahususi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuweka mikakati na kuchukua hatua mbalimbali za kisera, kisheria na kiutendaji kuimarisha sekta hii ya Bima.

Haya yanadhihirishwa na Dkt. Baghayo Saqware wakati alipozungumza na waandishi wa Habari mwezi Agosti 2025, Jijini Dar es salaam akisema

“Hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kimarisha Sekta ya Bima ni pamoja na kuteua Bodi ya Taifa ya Bima, ambapo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Mwenyekiti wa Bodi shupavu CPA Moremi Marwa akishirikiana na wajumbe, ameendelea kutoa dira, ushauri na miongozo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Bima nchini. Bodi ya Taifa ya Bima imekuwa kiungo muhimu katika kusimamia utekelezaji wa masuala ya Kisera na mikakati mbalimbali ya kukuza soko la bima nchini”. Alisema Dkt. Saqware.



Lakini pia Serikali ya Rais Samia imeongeza upatikanaji wa huduma bora za bima kwa wananchi, kwa kuvutia wawekezaji wapya na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa Sekta ya Bima. Mpaka kufikia Juni 2025 kuna ongezeko la Kampuni nne za Bima Mtawanyo ambazo kwa kiasi kikubwa zinamilikiwa na wawekezaji wageni kitu kinachochangia mapato ya nchi yetu na ongezeko la ajira kwa Watanzania.




Miongoni mwa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita pia ni kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya mwaka 2023 na Kanuni zake. Sheria hiyo ilipitishwa na Bunge na kusainiwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni hatua ya kihistoria inayolenga kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya kupitia mfumo wa bima. Kanuni na Miongozo ya Bima ya Afya kwa wote imeweka misingi ya utekelezaji, usimamizi, na ushirikishwaji wa wadau katika kuhakikisha huduma ya bima ya afya kwa kila Mtanzania inapatikana.

Vile vile kupitia uongozi madhubuti wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeendelea kuimarisha juhudi za utoaji wa elimu kwa umma, na hivyo TIRA kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima katika maisha ya kila siku ya wananchi na maendeleo ya taifa. Hii ikiambatana na kuanzisha miongozo na mikakati kwa ajili ya kuratibu shughuli za utoaji elimu na mawasiliano kwa umma ikiwemo Mpango Mkakati wa Mawasiliano wa TIRA (TIRA Communication Strategy) na Mpango wa Taifa wa Utoaji Elimu ya Bima (National Insurance Education Strategy).

Kuhamasisha Umma kuhusu dhana na umuhimu wa bima na kuimarisha mahusiano kupitia mikutano ya wadau mkoa kwa mkoa ambapo warsha, mikutano na semina zaidi ya 800 kupitia Kanda mbalimbali zimefanyika, vipindi vya redio zaidi ya 150, vipindi vya runinga zaidi ya 100 na habari za kwenye magazeti zaidi ya 100 kwa kipindi cha mwaka 2021-2025. Sekta ndogo ya bima imeendelea kutoa fursa mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.



vipindi vya runinga zaidi ya 100 na habari za kwenye magazeti zaidi ya 100 kwa kipindi cha mwaka 2021-2025. Sekta ndogo ya bima imeendelea kutoa fursa mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, imeendelea kuratibu na kushiriki kwenye matamasha ya kibiashara ya bima ndani na nje ya nchi. Matamasha hayo yamelenga kuhamasisha Umma kuhusu dhana na umuhimu wa bima, kujenga mahusiano ya kibiashara, na kufungua fursa mpya za uwekezaji katika Sekta ya Bima.

Si hivyo tu bali Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya maboresho katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 ambayo imeongeza wigo wa bima za lazima.

Hii ni katika maeneo muhimu ikiwemo bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi (imported goods) kuwa na bima za kampuni za ndani, majengo ya umma na biashara kuwa na bima, vivuko na pantoni kuwa na bima.

Aidha, Serikali imendelea kuhakikisha kuwa miradi yake mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa nchini, ikiwemo ya miundombinu, inakuwa na kinga ya bima kutoka kwenye kampuni za bima za ndani ili kulinda mali na uwekezaji unaofanywa na Serikali.

Kufuatia maboresho ya kisera na kisheria, idadi ya kampuni za bima na kampuni za bima mtawanyo (reinsurance) zimeongezeka nchini. Wawekezaji wapya wamevutiwa na mazingira bora ya ufanyaji wa biashara ya bima na uthabiti wa kiuchumi. Hatua hii inalinda uwekezaji wa Taifa na kuhakikisha kuna uendelevu wa miradi hiyo muhimu.

Kuanzishwa kwa Konsontia ya Bima ya Kilimo, kupitia ushirikiano na wadau, Serikali imeanzisha Konsotia ya Bima ya Kilimo kwa lengo la kuwahudumia wakulima, kupunguza athari za majanga ya asili, na kuongeza tija katika sekta ya kilimo. Hii ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa wakulima wanakuwa na uhakika wa kipato hata wanapokumbwa na majanga.

Pia kuanzishwa kwa Konsotia ya mafuta na gesi, ni eneo la kimkakati kwa uchumi wa nchi, imenufaika na uanzishwaji wa konsotia maalum ya bima inayolenga kusimamia vihatarishi na kulinda uwekezaji katika maeneo haya muhimu kwa uchumi wa nchi.

Uanzishwaji wa mifumo imeweka mazingira wezeshi yanayochochea matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa umma. Kupitia mazingira ya biashara yaliyoboreshwa, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetengeneza mfumo wa kidijitali wa usajili unaowawezesha wananchi na wawekezaji wanaotaka kutoa huduma za bima nchini kuweza kujisajili mahali popote walipo.

Akinukuliwa kwenye Mkutano wake na waandishi wa Habari, Dkt. Saqware amesema; "kupitia mfumo huo, waombaji wa usajili hawalazimiki kufika katika ofisi za TIRA, bali wanaweza kutuma maombi yao mtandaoni, kufuatilia hatua kwa hatua, na hatimaye kupata cheti cha usajili kwa njia ya kidijitali" Aliongeza kwa kusema; "Hatua hii imeongeza uwazi, kuondoa urasimu, kupunguza gharama na muda wa usajili, na kuimarisha utoaji wa huduma kwa kasi na ubora unaotarajiwa katika zama za kidijitali," .

Miongoni mwa Maagizo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Uunganishaji wa Taasisi za Serikali kupitia Mifumo ili iweze kusomana na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika miaka minne ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kumeimarishwa Mifumo ya TEHAMA kwa kutekeleza maagizo hayo, ambapo imefanikisha hatua kubwa ya kuunganisha mifumo ya TEHAMA na taasisi nyingine muhimu za Serikali.

Miongoni mwa taasisi zilizounganishwa ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mamlaka ya Usafiri Baharini (TASAC), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), na taasisi nyinginezo nyingi.




"Muunganiko huu wa mifumo umesaidia kuongeza uwazi, ufanisi wa usimamizi wa taarifa, urahisi wa kufuatilia mwenendo wa sekta ya bima, na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hatua hii ni ya kimkakati katika kujenga sekta ya bima inayozingatia matumizi ya teknolojia na inayoshirikiana kikamilifu na mifumo mingine ya kitaifa kwa maendeleo endelevu," alisema Dkt. Baghayo Saqware.

Halikadhalika, Sekta ya Bima bila kuathiri Imani, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imewezesha uanzishwaji wa huduma ya Bima ya Takaful ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaofuata misingi ya Kiislamu nao wanapata huduma za bima zinazozingatia imani zao na kusababisha ongezeko kubwa la watumiaji wa huduma za bima nchini. Hatua hii imepanua wigo wa ujumuishaji wa kifedha katika jamii kwa kuwa aina hiyo ya bima inawezesha makundi mbalimbali ya wananchi kutumia aina hiyo ya bima kulinda mali zao.

Hatua hizo mbalimbali zilizochukuliwa zimeimarisha sana Sekta ya bima na imepata mafanikio makubwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, ikiwa pamoja na kuongezeka kwa watoa huduma, ongezeko la ajira, wanufaika wa huduma, mali na mitaji ya bima kama takwimu zinavyoonesha:

Wakati mwaka 2021 watoa huduma ya bima walikuwa 993 lakini kufikia Juni 2025 wamefikia 2,425 Juni 2025, hii ikiwa ni sawa na wastani wa asilimia 22.1 kwa mwaka sawa na ongezeko la jumla ni asilimia 144.2.




Ukiona jinsi Sekta ya Bima inavyokuwa ni kutazama watoa huduma walioongezeka kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2021 hadi sasa, ambapo wapo watoa huduma za afya (HSPs), warekebishaji na watengenezaji magari (ARMs) na Watoa Huduma Kidijitali. Hapa pia unazungumzia kampuni za bima mtawanyo nchini zimeongezeka kutoka kampuni moja mwaka 2021 hadi kampuni nne mwaka 2025.

Wanufaika wa huduma za Bima walipoongezeka kutoka milioni 14.2 mwaka 2021 hadi kufikia milioni 25.9 mwaka 2024. Hii ina maana katika miaka minne kumekuwa na ongezeko la asilimia 82.4 ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 22.2 kwa mwaka. Hii imechangia kuzalisha ajira rasmi ndani ya Sekta ya Bima, kutoka wafanyakazi 3,527 mwaka 2021 hadi kufikia wafanyakazi 6,916 Juni 2025. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 96.1 na wastani wa ongezeko la asilimia 18.3 kwa mwaka hivyo kuwanyanyua kiuchumi Watanzania.

Kuna ongezeko pia la thamani ya mali katika soko la bima kutoka Shilingi trilioni 1.277 mwaka 2021 hadi kufikia Shilingi trilioni 2.340 mwaka 2024. Hii ni sawa na jumla ya ongezeko la asilimia 83.3, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 16.3 kwa mwaka.






# STAWI BOND YA TCB YAANDIKISHWA RASMI DSE




Hatifungani ya Stawi (Stawi Bond) ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB) imeandikishwa rasmi katika Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE).

Tukio hilo la kihistoria lilifanyika Desemba 3, 2025 kupitia hafla ya ugongaji kengele iliyoashiria kuorodheshwa kwake sokoni.

Uandikishwaji huo umefuatia tangazo rasmi la matokeo ya Stawi Bond lililotolewa na TCB chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mtendaji wake, Bw. Adam Mihayo, ambapo benki hiyo imeweka rekodi ya kuvuka lengo la ukusanyaji wa fedha kwa kiwango kikubwa.

Katika zoezi hilo, TCB ilikuwa imelenga kukusanya TZS 50 bilioni, lakini imefanikiwa kukusanya TZS 140.24 bilioni , sawa na asilimia 281 ya lengo la awali, ikiwa ni takribani mara tatu ya kiasi kilichokusudiwa.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, aliyemwakilisha Waziri wa Fedha, pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA Nicodemus Mkama.

Viongozi wengine waliokuwepo ni pamoja na Bw. Mecklaud Edson, Mkuu wa Idara ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Ndani aliyemwakilisha Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa Dar es Salaam, menejimenti na wafanyakazi wa TCB, CMSA na DSE, viongozi wa dini na serikali pamoja na wadau mbalimbali wa masoko ya mitaji.

Kutangazwa kwa matokeo ya Stawi Bond kulilenga kutoa taarifa ya jumla kuhusu kiasi cha fedha zilizokusanywa katika kipindi cha ununuzi wa hatifungani hiyo, pamoja na kiwango cha ushiriki wa wawekezaji, jambo linaloonesha imani kubwa ya umma katika TCB na soko la mitaji kwa ujumla.

Ufanisi huo unaifanya Stawi Bond kuwa miongoni mwa hatifungani zilizopata mafanikio makubwa katika soko la mitaji nchini, huku uorodheshwaji wake DSE ukitarajiwa kuongeza kina cha soko na kutoa fursa zaidi za uwekezaji kwa Watanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo CPA Mkama alisema " Benki ya TCB imeweka historia ya kuwa benki ya kwanza (1) inayomilikiwa na Serikali kwa hisa nyingi kuuza hatifungani kwa Umma na kupata mafanikio makubwa, na hatimaye leo hii inaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam".

# WATEJA WA ILIYOKUWA BENKI YA FBME WAANZA KUPOKEA ASILIMIA 30 YA FIDIA

Baadhi ya wateja wa iliyokuwa FBME Bank Limited (iliyo katika ufilisi) wameanza kupokea fidia ya ufilisi ya asilimia 30 iliyotangazwa hivi karibuni na Bodi ya Bima ya Amana (DIB).

Wateja hao, wameeleza hayo katika ujumbe wao kwa DIB wakielezea furaha yao baada ya kupokea fedha zao kwenye akaunti zao.

"Asante sana. Hela zimeingia muda si mrefu hapa. Nashukuru. Leo nitakula vizuri," ameeleza mteja mmoja (jina limefichwa) wa iliyokuwa benki ya FBME huko Mwanza baada ya kupokea malipo ya awamu ya tatu ya asilimia 30 katika akaunti yake.

Aidha, mnufaika mwingine wa fidia hiyo ya ufilisi ameeleza shukurani zake kwa wote ambao wamewezesha na wanawezesha kupatikana kwa fedha hizo zinazotokana na kufutiwa leseni FBME kutokana na kukiuka masharti ya leseni na kuwekwa chini ya ufilisi.

"Mi nashukuru na ninawashukuru sana kwa msaada wao na yeyote anayehusika kutupambania katika suala hili," amesema mnufaika mwingine (jina limefichwa) katika ujumbe wake kwa DIB.

DIB ilitangaza mapema wiki hii kuanza kwa mchakato wa kulipa fidia ya ufilisi awamu ya tatu ya asilimia 30 kwa wadai wa iliyokuwa benki ya FBME walioko Tanzania.

Malipo haya yanafanya wadai wa FBME nchini wawe wamelipwa jumla ya asilimia 85 ya madai yao, kwani katika awamu mbili za kwanza walilipwa jumla ya asilimia 55.

"Kutokana na tathmini iliyofanywa, DIB imeamua kulipa fidia ya ufilisi kwa wadai waliokuwa na amana zaidi ya TZS milioni 1,500,000.00 katika benki ya FBME kwa awamu ya tatu kwa upande wa wadai wa Tanzania pekee," alieleza Mkurugenzi Mkuu wa DIB, Bw. Isack Kihwili wakati anatangaza kuanza kulipwa fidia ya awamu ya tatu.

Kwa ujumla, wadai kwa upande wa Tanzania ni 1,414, ambao madai yao ya jumla kwa benki hiyo ni TZS bilioni 35.2; wadai wa kimataifa (TIB) wako 866 na madai yao ni TZS bilioni 308.22. Aidha, wateja wa tawi la Cyprus ni 5,480 wakidai jumla ya Euro milioni 1,254.62 (sawa na TZS milioni 3,596.00).

Malipo ya awamu nyingine yatategemea kiasi kitakachokusanywa ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa fedha zilizozuiliwa na mamlaka ya Marekani (FinCEN). Aidha, DIB kama mfilisi, itaendelea kufanya tathmini kadiri makusanyo yatakavyopatikana na kufanya malipo ya awamu nyingine kwa wadai pindi yatakapokuwa ya kuridhisha.

Benki Kuu ya Tanzania ilifuta leseni ya Benki ya FBME mwaka 2017 kutokana na kukiuka masharti ya leseni yake na kuichagua DIB kama Mfilisi. FBME ilikuwa na makao makuu yake hapa nchini na tawi nchini Cyprus. Hii imefanya zoezi la ufilisi kushirikisha mamlaka za Tanzania na Cyprus.



# BOT YARATIBU MIKUTANO YA KITAALAMU YA TEHAMA, UHASIBU KWA BENKI KUU ZA EAC

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeratibu mikutano miwili ya kitaalamu iliyowakutanisha wataalamu kutoka benki kuu za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) jijini Arusha.

Mikutano hiyo ni pamoja na ule wa Kamati ya Ufundi ya TEHAMA katika Masuala ya Fedha (MAC-IT Technical Workgroup) uliofanyika kuanzia Novemba 24 hadi 28, 2025 na Kamati ya Ufundi ya Uhasibu na Fedha (MAC – AF Technical Workgroup) ulioanza Desemba 1 hadi 4, 2025.

Ambayo yote ilifunguliwa na Meneja wa Idara ya Uchumi wa BoT – Tawi la Arusha, Bw. Aristides Mrema, kwa niaba ya Mkurugenzi wa tawi hilo.

Akizungumza katika mkutano wa TEHAMA Bw. Mrema alisema "Maendeleo ya kasi ya teknolojia, hususan matumizi ya Akili Unde (AI), yameleta fursa na changamoto mpya za kiusalama wa kimtandao, hivyo ni muhimu kwa benki kuu kuimarisha mifumo yao ya kujikinga na hatari hizo."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mifumo ya Mawasiliano wa BoT, Bw. Joel Ngussa, alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana uzoefu, kuimarisha ulinganifu wa usimamizi wa TEHAMA, na kuandaa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mifumo ya benki kuu wanachama.



Meneja wa Idara ya Uchumi Benki Kuu Tawi la Arusha, Bw. Aristides Mrema akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo.



Washiriki wa Mkutano wa Kamati ya Ufundi ya Tehama katika Masuala ya Fedha kwa Benki Kuu za nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika picha ya pamoja kabla ya kuanza kwa mkutano huo jijini Arusha.

Katika mkutano wa Kamati ya Ufundi ya Uhasibu na Fedha ulwashiriki walijadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo na uendelevu wa sekta ya fedha katika ukanda wa EAC.

Mada zilizojadiliwa ni pamoja na nafasi ya uhasibu katika ununuzi wa dhahabu ya fedha (Monetary Gold), matumizi ya Akili Unde (AI) katika uchanganuzi na usimamizi wa data za fedha, pamoja na mbinu bora za tathmini za uendelevu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Mikutano hiyo imeimarisha ushirikiano wa kikanda na kuonesha dhamira ya Benki Kuu ya Tanzania kuongoza mageuzi yanayolenga uthabiti, uwazi na uendelevu wa mifumo ya fedha



Washiriki wa Mkutano wa Kamati ya Ufundi ya Tehama katika Masuala ya Fedha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiendelea na majadiliano



Mkurugenzi wa Mifumo ya TEHAMA BoT, Bw. Joel Ngussa akitoa salamu za ukaribisho kwa washiriki wa mkutano huo kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

# BOT YAWANOA WANAFUNZI TAASISI YA UHASIBU ARUSHA






Meneja Msaidizi wa Usimamizi wa Mabenki Makubwa, Bw. Naiman Juwael, akizungumza katika mafunzo maalum kwa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Fedha na Benki kutoka Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA), yaliyofanyika Desemba 4, 2025, katika ukumbi wa chuo hiko.



Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendesha mafunzo maalum kwa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Fedha na Benki kutoka Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA), kwa lengo la kuongeza uelewa wao kuhusu masuala muhimu ya sekta ya fedha na kuwapa mtazamo wa moja kwa moja kuhusu namna tasnia hiyo inavyofanya kazi.

Mafunzo hayo, yaliyofanyika Alhamisi, Desemba 4, 2025, yalijumuisha mada mbalimbali kuhusu usimamizi wa taasisi za fedha, ikiwemo mabenki, pamoja na elimu juu ya uwekezaji katika dhamana za Serikali.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Meneja Msaidizi wa Usimamizi wa Mabenki Makubwa, Bw. Naiman Juwael, alisisitiza umuhimu wa mabenki kusimamiwa na kukaguliwa mara kwa mara ili kuhakikisha uthabiti wa sekta ya fedha unaendelea kuimarika.

Alieleza kuwa usimamizi madhubuti wa mabenki ni msingi muhimu katika kulinda uchumi wa nchi na maslahi ya wananchi.

"Benki Kuu inafanya jukumu hili la usimamizi wa mabenki na taasisi nyingine za fedha nchini kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha uthabiti wa sekta hii nyeti unakuwepo. Tunawapa elimu hii tukiamini kuwa ninyi ni wataalamu wajao wa sekta hii ya benki," alisema Bw. Juwael

Mafunzo haya ni sehemu ya jitihada endelevu za BoT katika kuwafikia wadau wake, hususan taasisi za elimu ya juu, kwa lengo la kuongeza ufahamu kuhusu majukumu yake, kukuza uelewa wa wanafunzi kuhusu masuala ya kifedha, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kitaaluma kati ya Benki Kuu na vyuo mbalimbali nchini.

# DUNIA *Kiganjani*

Dunia i kiganjani, kwa mifumo ya malipo,
Nyumbani hata njiani, unayafanya malipo,
Unafanya kwa amani, vile usalama upo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Una mahitaji yako, kutaka fanya malipo,
Pengine na simu yako, popote pale ulipo,
Fanya miamala yako, tena ni ya papo hapo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Tunazo nyingi kampuni, mawasiliano yapo,
Kwa hizohizo kampuni, miamala nayo ipo,
Utulie kivulini, TIPS ni mfumo upo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Mitandao mingimingi, na mifumo yao ipo,
TIPS yetu ya msingi, hapo utulivu upo,
Ndivyo twaupiga mwingi, huduma njema ziwepo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

TISS nao ni mfumo, huo pia wa malipo,
Benki na kampuni zimo, huko zafanya malipo,
Kwa uchumi msukumo, shughuli nyingi ziwepo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Pia mfumo mkuu, wa kibenki nao upo,
Mmiliki Benki Kuu, na watumiaji wapo,
Sana watuweka juu, wabunifu wetu wapo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Wataalamu tunao, na mifumo yetu ipo,
Wanafanya kazi hao, kufanya hiyo iwepo,
Utegemezi wa kwao, tunafanya usiwepo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Benki Kuu Tanzania, kuisimamia ipo,
Hata kutuandalia, na matumizi yawepo,
Pazuri tumefikia, na wa kujifunza wapo,
Ni mifumo wa malipo, ya Taifa Tanzania.

Wananchi himahima, mifumo mizuri ipo,
Ni mingi tena salama, na tena ya papo hapo,
Hebu itumie vema, maendeleo yawepo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Ndivyo yetu Tanzania, juu yataka iwepo,
Kuyafanya yenye nia, na unafuu uwepo,
Miamala kuingia, na kutoka papo hapo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

Mambo teknolojia, ndipo dunia ilipo,
Kwenda kidijiti pia, kuwa nyuma kusiwepo,
Benki Kuu Tanzania, mikakati mingi ipo,
Ni Mifumo ya Malipo, ya Taifa Tanzania.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**

**Limetolewa na Idara ya Mawasiliano**
**Benki Kuu ya Tanzania**

Anuani:
**Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete, 40184**
**S.L.P. 2303 Dodoma, Tanzania**
Barua pepe:
**botcommunications@bot.go.tz**
**info@bot.go.tz**
Tovuti:
**www.bot.go.tz**